



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

VOL. LXIII, No. 30

GAZETI

23 JULAI, 1982

BEI SH. 3/-

Linatelewa kwa Idhini ya Serikali na
Kuandikishwa Posta kama
Gazeti

DAR ES SALAAM

YALIYOMO

Taarifa ya Kawaida UK

Kuajiriwa na Kukabidhiwa Madaraka, n.k.	Na. 582	363
Notice <i>re</i> Supplements	Na. 583-4	364
Tanzia		364
Tangazo—Dhamana za Taifa	Na. 585	364
Uteuzi wa Mjumbe wa Baraza la Waku- rugenzi la Mamlaka ya Mkonge (TSA)	Na. 586	364
Kuteuliwa kwa Wajumbe wa KAMUS ya Wizara ya Maendeleo ya Utumishi na Uendeshaji Kazi	Na. 587	365
Kuandikishwa kwa Wahandisi	Na. 588	365
Wizara ya Kazi na Ustawi wa Jamii— Mgogoro wa Kazi	Na. 589	366

Taarifa ya Kawaida UA

Alama za Biashara	Na. 590	368
Kupotea kwa Hati za Kumliliki Ardhi	Na. 591-5	369
Kupotea kwa Hati za Bima	Na. 596-600	379
Uthibitisho na Usimamiaji wa Mirathi	Na. 601-7	370/71
Makampuni Yaliyofutwa katika Daftari la Makampuni	Na. 608	371
Jina la Biashara Lililofutwa kutoka katika Daftari la Majina ya Biashara	Na. 609	372
Hati za Uvumbuzi	Na. 610	372
Deed Poll Declaring Change of Name	Na. 611	372
Mali Isiyoye na Mwenyewe	Na. 612	372

KUAJIRIWA NA KUKABIDHIWA MADARAKA

TAARIFA YA KAWAIDA NA. 582

Ofisi ya Rais (Tume ya Kudumu ya Uchunguzi):

Kuwa Mchunguzi Msaidizi, Daraja la I:—
D. N. NGALAWA, Mchunguzi Msaidizi, Daraja la II,
kuanzia tarehe 1 Mei, 1982.

Wizara ya Maji na Nishati:

Kuwa Msaidizi Mhandisi Mtendaji:—
ALEX J. KAAVA, kuanzia tarehe 16 Juni, 1979.

Wizara ya Habari na Utamaduni:

Kuwa Maafisa Utamaduni Waandamizi, Daraja la II:—
J. MWAKIPESILE, Ofisa Utamaduni, Daraja la I, kuanzia tarehe 1 Mei, 1982.

PAULO RICHARD, Ofisa Utamaduni, Daraja la I, kuanzia tarehe 1 Mei, 1982.

LYAPA U. MATHIAS, Ofisa Utamaduni, Daraja la I, kuanzia tarehe 1 Mei, 1982.

J. S. MUGANGALA, Ofisa Utamaduni, Daraja la I, kuanzia tarehe 1 Mei, 1982.

Kuwa Ofisa Michezo, Daraja la III:—

C. J. KISABURI, Ofisa Michezo Msaidizi, kuanzia tarehe 1 Novemba, 1981.

Matangazo yahasuyo mali za watu waliofariki, kuvunja mikataba ya ushirikiano na mengineyo, yakiwa ya manufaa kwa umma yaweza kuchapishwa katika *Gazeti*. Matangazo yote yapelekwe kwa Mhariri, Idara ya Habari (Sehemu ya Uchapishaji), S.L.P. 9142, Dar es Salaam, Simu za Ofisi 31799 au 25375. *Kabla ya Jumanne ya kila Jama*. Matangazo yasipelekwe kwenye Wizara ya Maendeleo ya Utumishi Wala Idara ya Kupiga Chapa.

TAARIFA YA KAWAIDA NA. 583

Notice is hereby given that the following Acts were enacted by Parliament and are published in Acts Supplement No. 2 to *Gazette*, No. 30, Vol. LXIII, dated 23rd July, 1982:—

No. 5 of 1982.—An Act to apply a further sum of three hundred twenty-six million, nine hundred eighty-nine thousand, four hundred shillings out of the Consolidated Fund to the Service of the year ending on the thirtieth day of June, one thousand nine hundred and eighty-two and to appropriate the supply granted.

No. 6 of 1982.—An Act to apply a further sum of eight hundred eighty million, and seventy-one thousand, two hundred ninety-nine shillings out of the Consolidated Fund to the Service of the year ending on the thirtieth day of June, one thousand nine hundred and seventy-nine and to appropriate the supply granted.

No. 7 of 1982.—An Act to make better provisions for, and to consolidate laws relating to, local government, to repeal the Local Government Ordinance, to repeal certain other written laws and to provide for other matters connected with or incidental to the organization of local government in Mainland Tanzania.

No. 8 of 1982.—An Act to make better provision for the establishment of urban authorities for the purposes of local government, to provide for the functions of those authorities and for other matters connected with or incidental to those authorities.

No. 9 of 1982.—An Act to make provision for sources of revenue and the management of funds and resources of local government authorities and for other matters connected or incidental to securing the proper collection and sound management of Finances in the local government system.

No. 10 of 1982.—An Act to establish the Local Government Service Commission, and to make provisions relating to service in local government authorities and to other matters connected with or incidental to the service.

No. 11 of 1982.—An Act to repeal the Local Government Service (Negotiating Machinery) Act, 1963, and to make better provision for the participation of Workers in the settlement of disputes arising within the local government system and for other matters connected or incidental to the settlement of disputes in the local government service.

No. 12 of 1982.—An Act to amend the Decentralization of Government Administration (Interim Provisions) Act, 1972, in consequence of the re-establishment of local government authority.

No. 13 of 1982.—An Act to amend the National Industries (Licensing and Registration) Act, 1967.

No. 14 of 1982.—An Act to provide for the formation, constitution, registration and functioning of Co-operative Societies as instruments for the implementation of the policy of socialism and self-reliance; to repeal the Co-operative Societies Act, 1968 and the Jumuiya ya Washirika Act, 1979 and to provide for matters connected with those purposes.

No. 15 of 1982.—An Act to establish Co-operative audit, supervision and inspection of books of accounts its functions and to provide for matters related to audit, supervision and inspection of books of accounts of co-operative societies.

No. 16 of 1982.—An Act to amend the Tanzania Rural Development Bank, Act 1971 in order to allow the apex organization to subscribe for shares in the Bank.

TAARIFA YA KAWAIDA NA. 584

Notice is hereby given that an Order and Notices, as set out below, have been issued and are published in Subsidiary Legislation Supplement, No. 26, dated 23rd July, 1982, to this number of the *Gazette*:—

Order under the Interpretation of Laws and General Clauses Act, 1972 (Government Notice No. 94 of 1982).

Notice Under the Aerodromes (Licensing and Control) Act, 1974 (Government Notice No. 95 of 1982).

Notice Under the National Defence Act, 1966 (Government Notice No. 96 of 1982).

TANZANIA

Mtukufu Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, anasikitika kutangaza kifo kilichotokea katika Hospitali ya Muhimbili kwa kuanguka ghafla tarehe 1 Aprili, 1982 cha D.183 LAURENT MLIMAKIFU, askari wa kawaida wa Jeshi la Polisi Tanzania, Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi.

TAARIFA YA KAWAIDA NA. 585

TANGAZO

DHAMANA YA TAIFA

6½% Tanzania Stock 1983/84

6½% Tanzania Registered Stock "B" 1981/84

7½ Tanzania Stock 1995

Malipo ya faida ya dhamana zilizotajwa hapo juu yatafanywa tarehe 1 Septemba, 1982 kwa ajili ya utayarishaji wa hundi za malipo ya faida, vitabu vya uandikishaji wa dhamana hizo vitafungwa tarehe 31 Julai, 1982 jioni na baada ya siku hiyo dhamana zitauzwa ama kununuliwa bila malipo ya faida.

Benki Kuu ya Tanzania,
Idara ya Dhamana za Taifa,
S.L.P. 2939,
DAR ES SALAAM

TAARIFA YA KAWAIDA NA. 586

UTEUZI WA MJUMBE WA BARAZA LA WAKURUGENZI LA MAMLAKA YA MKONGE (TSA)

Inatangazwa kuwa kwa mujibu wa Kifungu Na. 1 (i) (b) cha jedwali ya Sheria ya Mkonge (The Sisal Industry Act, 1973) na 2 ya 1973 Waziri wa Kilimo, Nd. J. B. MACHUNDA amemteua Nd. A. TORRIANI kuwa mjumbe wa Baraza la Wakurugenzi la Mamlaka ya Mkonge, bada'a ya Meneja wa Biashara za Nje (Import/Export Dept.) wa Benki Kuu.

Uteuzi wa Nd. TORRIANI ni kuanzia tarehe 1 Julai, 1982 na utaendelea hadi tarehe 31 Mei, 1985.

Taarifa hii inasahihisha Taarifa ya Kawaida Na. 472 iliyotolewa katika gazeti la tarehe 18 Juni, 1982.

Wizara ya Kilimo,
5 Julai, 1982

C. K. TUPA.
k.n.y. Katibu Mkuu

TAARIFA YA KAWAIDA NA. 587

KUTEULIWA KWA WAJUMBE WA KAMUS YA WIZARA YA MAENDELEO YA UTUMISHI NA UENDESHAJI KAZI

Wajumbe wafuatao wameteuliwa kuwa wajumbe wa KAMUS ya Wizara ya Maendeleo ya Utumishi na Uendeshaji Kazi kuanzia tarehe 17 Juni, 1982 kwa muda wa miaka mitatu.

- (1) Nd. P. Y. Ngw'andu (Mb.), Waziri—Mwenyekiti.
- (2) Nd. B. Mulokozi, Katibu Mkuu—Katibu.
- (3) Nd. M. P. Lukindo (Bibi) Mjumbe.
- (4) Nd. E. R. Mayowera Mjumbe.
- (5) Nd. B. B. C. Mumwi Mjumbe.
- (6) Nd. T. S. N. Mgawe Mjumbe.
- (7) Nd. Maria Leo (Bi.) Mjumbe.

A. H. P. KAIZA,
k.n.y. Katibu Mkuu

Dar es Salaam, Wizara ya Maendeleo ya Utumishi
9 Julai, 1982 na Uendeshaji Kazi

TAARIFA YA KAWAIDA NA. 588

KUANDIKISHWA KWA WAHANDISI

The Engineers Registration Act

Wahandisi wafuatao wameandikishwa chini ya Sheria Na. 49 ya Uandishi Wahandisi ya mwaka 1968:

No. 290.

Full Name: MATHEW B. MUNYAGI.

Qualification: B.Sc. (Electrical Eng.), University of Nairobi.

Present address: P.O. Box 104, Dar es Salaam.

Status and date of registration: Fully Registered Engineer with effect from 18th September, 1981.

Fees: Tanzania Shs. 100/-.

No. 291.

Full Name: A. C. BUKANGWA.

Qualification: B.Sc. (Civil Eng.), University of Science and Technology: Kumasi, Ghana.

Present address: P.O. Box Dar es Salaam.

Status and date of registration: Fully Registered Engineer with effect from 18th September, 1981.

Fees: Tanzania Shs. 100/-.

No. 292.

Full Name: GOPINATH V. SAVANT.

Qualification: B.E. (Civil Eng.), University of Karnataka, India.

Present address: P.O. Box 2657, Dar es Salaam.

Status and date of registration: Fully Registered Engineer with effect from 18th September, 1981.

Fees: Tanzania Shs. 100/-.

No. 293.

Full Name: SIMON W. SUMARI.

Qualification: B.Sc. (Civil Eng.), University of Nairobi.

Present address: P.O. Box 1283, Dar es Salaam.

Status and date of registration: Fully Registered Engineer with effect from 18th September, 1981.

Fees: Tanzania Shs. 100/-.

No. 294.

Full Name: SAJJAD A. VERSI.

Qualification: B.Sc. (Civil Eng.), University of Nairobi.

Present address: P.O. Box 1924, Dar es Salaam.

Status and date of registration: Fully Registered Engineer with effect from 18th September, 1981.

Fees: Tanzania Shs. 100/-.

No. 295.

Full Name: A. V. GEORGE.

Qualification: Diploma (Civil Eng.).

Present address: P.O. Box 104, Dar es Salaam.

Status and date of registration: Fully Registered Engineer with effect from 18th September, 1981.

Fees: Tanzania Shs. 100/-.

No. 296.

Full Name: K. A. PARPIA.

Qualification: B.Sc. (Civil Eng.), University of Bhopal, India.

Present address: P.O. Box 1984, Moshi.

Status and date of registration: Fully Registered Engineer with effect from 18th September, 1981.

Fees: Tanzania Shs. 100/-.

No. 297.

Full Name: C. L. MUGINI.

Qualification: B.Sc. (Civil Eng.), University of Dar es Salaam.

Present address: P.O. Box 6904, Dar es Salaam.

Status and date of registration: Fully Registered Engineer with effect from 20th November, 1981.

Fees: Tanzania Shs. 100/-.

No. 298.

Full Name: JUSTIN A. LYATUU.

Qualification: B.Sc. (Mech. Eng.), University of Nairobi. M.Sc. (Airport Transport) U.K.

Present address: P.O. Box 4915, Dar es Salaam.

Status and date of registration: Fully Registered Engineer with effect from 20th November, 1981.

Fees: Tanzania Shs. 100/-.

No. 299.

Full Name: SUEB R. MPINZIRE.

Qualification: M.Sc. (Civil Eng.), Warsaw University. Ph.D. (Structural Eng.), Warsaw University, U.S.S.R.

Present address: P.O. Box 35131, Dar es Salaam.

Status and date of registration: Fully Registered Engineer with effect from 20th November, 1981.

Fees: Tanzania Shs. 100/-.

No. 300.

Full Name: GORDIAN R. KANKIKO.

Qualification: B.Sc. (Electrical Eng.), University of Dar es Salaam.

Present address: P.O. Box 7292, Dar es Salaam.

Status and date of registration: Fully Registered Engineer with effect from 20th November, 1981.

Fees: Tanzania Shs. 100/-.

No. 301.

Full Name: IKETI P. T. SHALI.

Qualification: B.Sc. (Engineering) University of Dar es Salaam.

Present address: P.O. Box 9470, Dar es Salaam.

Status and date of registration: Fully Registered Engineer with effect from 20th November, 1981.

Fees: Tanzania Shs. 100/-.

No. 302.

Full Name: PULLANIKATIL RAJAGOPALAN.

Qualification: B.Sc. (Civil Eng.), University of Kerala, India.

Present address: P.O. Box 21011, Dar es Salaam.

Status and date of registration: Fully Registered Engineer with effect from 22nd April, 1981.

Fees: Tanzania Shs. 100/-.

No. 303.

Full Name: RODNEY J. CAPPER.

Qualification: B.Sc. (Civil Eng.), University of Glasgow, U.K.

Present address: P.O. Box 2555, Dar es Salaam.

Status and date of registration: Fully Registered Engineer with effect from 14th May, 1982.

Fees: Tanzania Shs. 100/-.

No. 304.

Full Name: MUNAVER M. VALJI.*Qualification:* B.Sc. (Civil Eng.), Cardiff University, U.K.*Present address:* P.O. Box 564, Dar es Salaam.*Status and date of registration:* Fully Registered Engineer with effect from 14th May, 1982.*Fees:* Tanzania Shs. 100/-.

No. 305.

Full Name: ANAMALAI SORNALINGAM.*Qualification:* B.Sc. (Civil Eng.), University of Madras, India.*Present address:* P.O. Box 3385, Dar es Salaam.*Status and date of registration:* Fully Registered Engineer with effect from 14th May, 1982.*Fees:* Tanzania Shs. 100/-.S. MOLLEL (MRS.),
Secretary
Engineers Registration Board**TAARIFA YA KAWAIDA NA. 589****WIZARA YA KAZI NA USTAWI WA JAMII
MGOGORO WA KAZI**

Na. 17/1980

baina ya

**JUMUIYA YA WAFANYAKAZI TANZANIA
(JUWATA)**

(Kwa niaba ya Wanachama wao)

na

**KARSAN RAMJI PATEL & COMPANY LIMITED
DAR ES SALAAM****Mahakama ya Kazi:**

J. J. M. MACKANJA, Naibu Mwenyekiti.

B. MAHARAGE JUMA, Mshauri A.T.E.

H. S. KIPACHA, (Mshauri)—JUWATA—Hayupo.

Mwakilishi wa JUWATA:

M. E. KALUWA, Katibu, Makao Makuu (Akiwakilishwa na Nd. YOHANE ALMASI).

Walalamikaji:

Baadhi yao wapo.

Kuwakilisha Waajiri:

KARSAN PATEL, Mkurugenzi.

UAMUZI

Kama alivyosema Ndugu Kaluwa katika hoja zake za mwisho, mgogoro huu ni wa aina ya pekee na haupo mwingine ambao unafanana nao. Yapo mambo mawili makubwa ambayo yanaufanya kuwa na hali hiyo: kwanza, katika migogoro yote ya nyuma watu ambao wamekuwa wakidai kurudishwa kazini wamekuwa ni wafanyakazi wa kudumu. Pili, katika migogoro ya nyuma, tofauti na huu, wafanyakazi wamekuwa wakilalamikia ama kuachishwa au kufukuzwa kazi na hapa wafanyakazi wasio wa kudumu wanadai ovataimu na baadhi yao wanataka warudishwe kazini. Baada ya kutafakari hoja hizo kwa makini sana pamoja na ushahidi uliotolewa, washauri wameshindwa kuafikiana kuhusu mambo haya muhimu. Sasa ufuatao ndio uamuzi wa Mahakama.

Haupo ubishi kwamba mgogoro huu ni wa siku nyingi. Walalamikaji wamekuwa wakikwama hapa na pale. Wakati mwingine wamelazimika kulalamikia Ikulu wa Kitaka kumuona Rais. Wameyafikisha malalamiko yao mbele ya Chama baada ya kuona kwamba JUWATA. Wilayani na Mkoani ilikuwa haiwatendei haki. Kutoka Ikulu walielekezwa kumuona Katibu Mkuu wa JUWATA na hatimaye mgogoro huu umetufikia hapa Mahakama ni kwa ajili ya uamuzi wa mwisho.

Kulingana na ushahidi uliopo imedhihirika kwamba walalamikaji wote wamepata kuwa wafanyakazi wa Kampani moja ya Ujenzi ijulikanayo kama Karsan Ramji Patel & Company Limited. Wachache wao ama wameachishwa au wamefukuzwa kazi. Wale ambao bado ni wafanyakazi pamoja na wale walioachishwa au kufukuzwa kazi wamekuwa ni vibarua isipokuwa wachache tu ndio wamefanywa wafanyakazi wa kudumu.

Chanzo kikubwa cha mgogoro huu si madai ya wafanyakazi kwamba sasa wote wanufaike na masharti ya kudumu. Dai lao kubwa linahusu mapunjo ya malipo ya ovataimu kwa masaa ya ziada wanayodai walifanya kazi lakini hawakulipwa. Awali kabisa walidai saa mbili za ziada kwa kila siku za kawaida na Jumapili au sikukuu za Taifa, na saa 3½ za ziada kwa kila Jumamosi. Kikao baina yao na Mwajiri kilipoitishwa na Ndugu Mjema wa kutoka Ofisi ya JUWATA ya Wilaya, walalamikaji walidai nusu saa tu kwa kila siku za kawaida, saa 3½ kwa kila Jumamosi na saa 16 kwa siku za sikukuu na Jumapili. Walidai pia likizo kwa wote wote waliokwisha maliza mwaka kazini. Hata hivyo, katika maoni yake Ndugu Mjema alisema kwamba walalamikaji hawakusitahili likizo kwa kuwa hapakuwa na mtu ye yote kati yao ambaye alikuwa amemaliza siku 280 mfululizo akiwa kazini kwa kuwa walikuwa ni vibarua. Kuhusu saa za ziada Ndugu Mjema aliona kwamba hawakuwa na haki hiyo kwa kuwa walikuwa wakifanya kazi kwa muda wa saa 8 tu kutwa, na kila walipozidi muda huo walilipwa ovataimu (Kielelezo JUWATA Na. 2).

Walalamikaji hawakuukubali ushauri huo. Hivyo walielezea JUWATA Mkoani ambako walirudishwa kwa Ndugu Maembe. Ndugu Maembe aliafikiana na uamuzi wa Ndugu Mjema. Hata Ndugu Marenda, aliyekuwa Katibu wa JUWATA wa Mkoa, alikubaliana na maoni ya wenzake. Kwa ajili hiyo aliwapeleka walalamikaji kwa Afisa Kazi Mwandamizi kulingana na Kielelezo cha JUWATA Na. 3. Hata huko walalamikaji hawakuona kwamba walitendewa haki, wakiwa wanawashtumu viongozi hao wa JUWATA na Afisa Kazi Mwandamizi kwamba walikuwa wakilandika mambo tofauti na yale wao walivyosema au yale Mwajiri wao aliyokiri mbele ya vikao mbali mbali. Kutokana na ushahidi aliokusanya, Ndugu Mboggo, Afisa Kazi Mwandamizi, aliona kwamba walalamikaji hawakuwa na sitahili yo yote juu ya ovataimu. Katika ushauri wake uliomo katika Aya ya mwisho ukurasa wa pili wa kielelezo cha JUWATA Na. 6 Ndugu Mboggo alipoyakataa madai haya alisema:—

“Walalamikaji wanakubali kwamba siku yo yote (sic) wafanyapo ovataimu hulipwa na hapana ye yote aliewahi (sic) kufanya ovataimu kisha asipate malipo yake.

Hii ina maana kwamba kila wanapofanya ovataimu walikuwa wakilipwa kama kumbukumbu za tajiri alizozionyesha ofisini hapa zilivyokuwa zinaonekana”

Upo ukweli kwamba walalamikaji walikuwa wakilipwa ovataimu. Ushahidi ulivyo, na jinsi walalamikaji wanavyokubali, ni kwamba ovataimu hiyo ilikuwa inalipwa kwa kazi iliyofanywa baada ya muda wa kumaliza kazi. Saa ya kumaliza kazi ilikuwa ni saa 10.00 kila siku, walivyofanya kazi. Hapo haupo ubishi kabisa.

Ubishi uliopo ni saa ya kuanza kazi na idadi ya saa walizofanya kazi. Walalamikaji wanadai kwamba kazi walikuwa wanaanza saa 1.30 asubuhi kila siku na kumaliza kazi yao saa 10.00. Iwapo walienda kufanya kazi baada ya saa 10.00 basi walilipwa ovataimu.

Lakini tukichukuwa kwamba walianza kazi saa 1.30 hadi saa 10.00, basi huo ni muda wa saa 8½ kila siku. Kwa kuwa muda wa kufanya kazi ni saa 8.00 tu kutwa, basi walikuwa wanayo ziada ya ½ saa kila siku. Ni hii nusu saa ambayo walalamikaji wamekuwa wakidai bila mafanikio. Wamedai kwamba katika uchunguzi mbali mbali uliofanywa na viongozi wa ngazi zilizohusika wote waliohojiwa walisema kwamba walikuwa wakianza kazi saa 1.30 asubuhi. Hata mwajiri anadaiwa kukubali mbele ya vikao mbali kwamba walalamikaji walianza kazi saa 1.30. Lakini taarifa za maandishi za vikao hivyo, ambazo ni pamoja na vielelezo vya JUWATA Na. 2, Na. 6, vinaonyesha kwamba mwajiri alisema kwamba kazi ilikuwa inaanza saa 2.00 asubuhi. Wamedai hapa kwamba mbinu zilitumiwa ili kufifilisha madai yao kwa kutoa taarifa ambazo si za kweli, na huenda ndiyo maana wanajiona hawakutendewa haki kote walikopitia.

Katika ushahidi uliotolewa hapa imedhihirika kwamba wale ambao walikuwa wanakaa mbali na sehemu ambayo mwajiri alikuwa akifanya kazi ya ujenzi, walitakiwa, na walifanya hivyo, kuripoti nyumbani kwa mwajiri kati ya saa 1.15 na saa 1.30. Kutoka nyumbani kwa mwajiri walichukuliwa na gari la mwajiri hadi mahali ujenzi ulikuwa ukifanywa ambako ni pamoja na Mwananyamala, Mavuno House, Kunduchi na kadhalika. Wale waliokuwa wanakaa jirani na sehemu ya ujenzi walikuwa wakienda kwa mguu. Ndugu Athumani Omar (Shahidi wa kwanza wa upande wa wafanyakazi) ameongeza kusema kwamba hapo nyumbani kwa mwajiri walikuwa hawaitwi majina. Kulingana na ushahidi huu hoja kubwa inayojitokeza kwa uamuzi ni moja tu, nayo inakuwa ni swali hili: Je, walalamikaji walianza kazi saa ngapi?

Ndugu Mjema, Ndugu Maembe, Ndugu Marenda, Ndugu Mboggo na Ndugu Maenda wanakubaliana katika maoni yao kwamba walalamikaji walishindwa kuyathibitisha madai yao na kwamba walilipwa ovataimu kwa saa zote za ziada walizofanya kazi. Ndugu Ochieng', aliyeteuliwa kushughulikia suala hili lilipofikishwa JUWATA Makao Makuu naye hakupata ufumbuzi wa suala hili, bali alisema:—

“Dai la ovataimu halikukubalika kwa sababu haikupatikana kumbukumbu inayoonyesha kiasi cha ovataimu zilizofanywa na lini ovataimu hizi zilifanyika. Walidai kwamba walikuwa wakifanya saa 8½ badala ya saa 8:00 (nane kamili) lakini rekodi aliyonyesha mwajiri ilionyesha kwamba alikuwa akilipia ovataimu ambazo zilizidishwa na mfanyakazi yeyote zaidi ya masaa 8.”

Kwa kuwa ilionekana kwamba ulikuwapo ubishi juu ya masaa ya kazi Ndugu Ochieng' alikubaliana na mwajiri—

“..... kwamba Mwajiri na JUWATA Wilayani watatengeneza mkataba wa pamoja ambao utakuwa unapanga saa za kazi na masharti mengine ya hali bora za kazi pamoja na mshahara ili kuondoa tatizo la kufanya kazi bila saa maalum”.

Mahakama inakubaliana na maono ya Ndugu Ochieng' kwamba lilikuwapo tatizo la saa maalum za kuanza kufanya kazi. Hata ushahidi wa Ndugu Athumani Omari unaelekea kuyaunga mkono mealezo haya aliposema:—

“..... Tuliokuwa tunafanya kazi mbali Kunduchi tulikuwa tunapeleka kwa gari na wale wa sehemu za jirani walikwenda kwa miguu..... Kwa kuwa tulikuwa tunapita sehemu mbali mbali tulikuwa tunafika saa mbili hivi.”

Mwajiri amesema waliweza kuchelewa kufika hadi saa 2.15 au saa 2.30. Ni wakati ambapo mlalamikaji au foreman wake alipokuwa anafika sehemu ya ujenzi ndipo alipopanga kazi siku hiyo, wala hayupo mlalamikaji anayedai kwamba mara tu baada ya kufika kwenye sehemu ya kazi kabla ya kufika mwajiri au foreman wake, alianza kazi bila ya kupangiwa kwanza. Huenda ndiyo maana Ndugu Maharage Juma, mshauri wa upande wa waajiri, ameona kwamba saa ya kazi haikuwanzwa kabla ya kufika sehemu ya ujenzi.

Mimi ninakubaliana na maoni haya kwa sababu kubwa mbili. Kwanza hakuna aliyekuwa na kazi maalum ya kufanya kila siku kwa kuwa walalamikaji walikuwa wakipangiwa kazi baada ya kufika kwenye sehemu zao za kazi. Pili, pale nyumbani kwa mwajiri wao hapakuwa mahali pao pa kazi na walalamikaji wote wanajua hivyo, ndiyo maana baadhi yao ambao walikuwa wanaisi jirani na sehemu za ujenzi hawakutakwa kufika nyumbani kwa mwajiri. Kama tutakubaliana na madai ya walalamikaji kwamba walikuwa wanaanza kazi mara tu baada ya baadhi yao kufika nyumbani kwa mwajiri, basi haipo sababu kwa nini hawakudai ovataimu kwa muda wote baada ya saa 10.00 walipomaliza kazi hadi saa ile waliporudi nyumbani kwa mwajiri kabla ya kurudi majumbani kwao jioni. Mahakama imeona kwamba kule kufika nyumbani kwa mwajiri ilikuwa ni kupewa usafiri ili wafike mahali pao pa kazi mapema. Ni kwa ajili hiyo hiyo mashirika ya umma pamoja na makampuni ya umma au ya watu binafsi yaliyowajengea wafanyakazi nyumba za kuishi hutoa usafiri kutoka sehemu hizi hadi mahali pao pa kazi ili wafanyakazi wafike mapema hata kabla ya saa ya kuanza kazi kutimia. Litakuwa jambo lisi la kawaida iwapo wafanyakazi hao watageuka na kusema wameanza kazi mara tu baada ya kupanda gari la mwajiri wao au mara tu baada ya kufika kazini kabla ya saa ya kazi kutimia. Kwa jinsi hali ilivyo, mwajiri katika mgogoro huu alikuwa akitoa huduma tu kwa wafanyakazi kama waajiri wengine wanavyofanya.

Walakini wadai wamesisitiza kwamba baada ya kuona kwamba alikuwa akiwapunja, mwajiri alibadili saa za kazi kwa kuishia saa 9.30 alasiri. Huenda ikawa hivyo, lakini haupo ushahidi wote wa kulithibitisha dai hili. Kwa hiyo Mahakama imeridhika kwamba walalamikaji walilipwa kwa kazi waliyofanya kuanzia saa 2.00 hadi saa 10.00, na walilipwa ovataimu baada ya saa 10.00. Madai ya mwajiri kwamba alwapa nusu saa ya chakula si ya kweli kwa sababu haupo ushahidi wa kuyathibitisha.

Kuhusu madai ya JUWATA kwamba vibarua wali-onyimwa kazi wanudishwe kazini hayana msingi wote wa kisheria. Kama alivyosema Ndugu Maenda katika maoni yake (MWAJIRI Na. 2) kwa kuwa walalamikaji ni vibarua wanaweza kupunguzwa wakati wote kazi zinapopungua. Kisheria mkataba baina ya kibarua na mwajiri unamalizika kila siku baada ya mfanyakazi huyo kulipwa ujira wake jioni. Kwa hali hii ni juu ya mwajiri kukubaliana na mfanyakazi kibarua kuingia mkataba kila siku kabla ya kuanza kazi. Mkataba huu si wa maandishi, bali ni wa makubaliano ya mdomoni tu.

Suala la kodi ya mapato halituhusu sisi kama Mahakama ya Kazi. Walalamikaji wanaweza kupata ushauri moja kwa moja kutoka Idara ya Kodi ya Mapato. Na suala la kuwajiri wafanyakazi kwa masharti ya muda wa kudumu linategemea uwezo wa JUWATA kuinga mkataba wa mwajiri kama walivyopendekeza katika kikao baina ya JUWATA (Ndugu Ochieng') na mwajiri. Viningevyo madai ya ovataimu na kuajiriwa kwa walalamikaji yanakataliwa; na yamekataliwa.

Uamuzi huu umetolewa hadharani leo tarehe 21 Julai, 1981 na unakuwa na nguvu mara moja.

Dar es Salaam,
21 Julai, 1981

J. J. M. MACKANJA,
Naibu Mwenyekiti,
Mahakama ya Kazi

TAARIFA YA KAWAIDA NA. 590

ALAMA ZA BIASHARA
Sheria ya Alama za Biashara
(Sura ya 394)

Kwa wote mnaohusika:—

Juani kwamba yamefanywa maombi ya watu wanaotajwa humu ya kutaka kuandikishwa Alama za Biashara zifuatazo zitakazotumika kwa ajili ya bidhaa za aina mbali mbali kama inavyoonyeshwa kwenye Nyongeza ya III ya Kanuni za Alama za Biashara za mwaka 1958.

Mtu ye yote mwenye sababu ya kupinga moja au zaidi ya moja ya alama hizo anaweza kutoa taarifa ya kupinga kwa kutumia fomu maalum kabla ya siku sitini hazijapita kuanzia tarehe ya Gazeti hili.

Muda wa kutoa taarifa ya kupinga unaweza kuongezwa na Msajili iwapo ataona yafaa kwa masharti atakayo- yaweka.

Upingaji rasmi usipelekwe mpaka kwanza muombaji awe amepelikwa taarifa kwa barua ili apewe nafasi ya kufuata hiyo Alama yake kabla ya kupatikana gharama ya kutayarisha taarifa ya kupinga. Iwapo muombaji hakupelekwa taarifa hiyo, basi mpingaji hataweza kupata hukumu ya kulipa gharama.

Sampuli ya Alama hizo zilizoombwa kuandikishwa zinaweza kuonekana kwenye Ofisi ya Msajili wa Alama za Biashara, Dar es Salaam.

Dar es Salaam,
14 Julai, 1982

C. NINDI,
Msajili Msaidizi wa Alama
za Biashara

15830

Sehemu A DARAJA LA 31



Kielelezo cha bidhaa: Kuku na mabata hai na wanyama na ndege hai wakuwinda.

Jina la kampuni: Imperial Foods Limited (Kampuni ya Kiingereza) Watengenezaji na wafanya biashara.

Anuani: Rose House, Grimsby Lincolnshire, England.

Mwakilishaji: Abdul Malik & Surendra, S.L.P. 1132, Dar es Salaam.

Tarehe: 25 Machi, 1975.

Sharti: Uandikishaji wa alama hii ya biashara hautoi kibali cha pekee cha utumizi wa neno "ROSS".

16846

Sehemu A DARAJA LA 1



Kielelezo cha bidhaa: Madawa yatumiwayo kwenye viwanda, mashamba, bustani kutia ngozi zisioze; gundi, vifaa vyenye gundi vitumiwavyo viwandani.

Jina la kampuni: Henkel KGaA, Kampuni ya Kijerumani, Watengenezaji.

Anuani: Henkelstrasse 767, Dusseldorf—Holthausen, Germany.

Mwakilishaji: Donaldson and Wood, S.L.P. 176, Dar es Salaam.

Tarehe: 5 Agosti, 1977.

Sharti: Alama hii ya biashara ishirikiane na alama za biashara namba 16847, 10394, 10395, 10396, 16006, 16007, 16009 na 16010.

16847

Sehemu A DARAJA LA 16

Kielelezo cha bidhaa: Makaratasi na vifaa vitengenezwa- vyo kutokana na makaratasi, karatasi nene kama ubao na vifaa vyake, makaratasi yaliyochapishwa, vifaa vitumi- wavyo ofisini, Gundi, Gundi za makaratasi vifaa vya nyu- mbani, shule na matumizi ya ofisini.

Jina la kampuni: Henkel KGaA, Kampuni ya Kijerumani, Watengenezaji.

Anuani: Henkelstrasse 767, Dusseldorf—Holthausen, Germany.

Mwakilishaji: Donaldson and Wood, S.L.P. 176, Dar es Salaam.

Tarehe: 5 Agosti, 1977.

Sharti: Alama hii ya biashara iandamane na alama za biashara nambari 16846, 10395, 10396, 16006, 16007, 16009 na 16010.

16577

Sehemu A DARAJA LA 32
NORDLIGHT

Kielelezo cha bidhaa: Pombe za Kizungu, Divai nye- kundu, vinywaji visivyoleweshwa na vifaa ya matayarisho yake.

Jina la kampuni: Herm G. Dethleffsen, (Kampuni inayo- endeshwa kwa mujibu wa sheria za Germany) Watenge- nezaji na wafanya biashara.

Anuani: 2390 Flensburg Schleswiger Str. 107, Federal Republic of Germany.

Mwakilishaji: Donaldson and Wood, Mwakili, S.L.P. 176, Dar es Salaam.

Tarehe: 20 Januari, 1977.

Sharti: Alama hii ya biashara ishirikiane na alama ya biashara Nambari 16584.

16596

Sehemu A DARAJA LA 34
GALLAHER

Kielelezo cha bidhaa: Tumbaku, Tumbaku iliyosindi- kwa, vivutio, kama inavyoonyeshwa kwenye daraja la 34. na viberiti.

Jina la kampuni: Gallaher Limited (Kampuni ya Kiingereza) watengenezaji na wafanya biashara.

Anuani: Virgina House, 134/148 York Street, Belfast, Northern Ireland.

Mwakilishaji: Donaldson and Wood, Mwakili, S.L.P. 176, Dar es Salaam.

Tarehe: 29 Januari, 1977.

18851 Schemu A DARAJA LA 5

NORIDAY

Kielelezo cha bidhaa: Bidhaa zote zilizomo katika daraja la 5.

Jina la kampuni: Syntex Corporation (Watengenezaji).

Anuani: Bank of America Building, Calle 50, Panama, Republic of Panama.

Mwakilishaji: Donaldson and Wood, Mwakili, S.L.P. 176, Dar es Salaam.

Tarehe: 10 Desemba, 1981.

TAARIFA YA KAWAIDA NA. 591

KUPOTEA KWA HATI YA KUMILIKI ARDHI

Sheria ya Uandikishaji wa Ardhi

(Sura ya 334)

Hati nambari: 12643.

Miliki aliyeandikishwa: BENJAMINI MANGO.

Ardhi: L.O. No. 17954 Kiwanja Na. 112 Kitafu "J" kilichopo Magomeni Wilaya ya Kinondoni Jijini Dar es Salaam.

Eneo: 3,430 Futi za Mraba.

Taarifa imetolewa kwamba Hati ya Kumiliki ardhi iliyotajwa hapo juu imepotea na ninakusudia kutoa hati mpya badala yake iwapo hakuna kipingamizi kwa muda wa miezi miwili tokea tarehe ya taarifa hii.

Hati ya asili ikionekana, lazima irudishwe kwa Msajili wa Hati, Idara ya Hati za Ardhi, S.L.P. 1191, Dar es Salaam, au kwa Kamishna wa Wilaya.

Dar es Salaam,
13 Julai, 1982

A. M. A. OMAR,
Msajili wa Hati

TAARIFA YA KAWAIDA NA. 592

KUPOTEA KWA HATI YA KUMILIKI ARDHI

Sheria ya Uandikishaji wa Ardhi

(Sura ya 334)

Hati nambari: 15556.

Miliki aliyeandikishwa: HERBERT KIMBERWA KATUA NA EMMANUEL GEORGE YOHANA KAMA WADHAMINI.

Ardhi: L.O. No. 21483 Kiwanja Na. 389 kilichopo Msasani Jijini Dar es Salaam.

Eneo: 26,540 Futi za Mraba.

Taarifa imetolewa kwamba Hati ya Kumiliki Ardhi iliyotajwa hapo juu imepotea na ninakusudia kutoa hati mpya badala yake iwapo hakuna kipingamizi kwa muda wa miezi miwili tokea tarehe ya taarifa hii.

Hati ya asili ikionekana, lazima irudishwe kwa Msajili wa Hati, Idara ya Hati za Ardhi, S.L.P. 1191, Dar es Salaam, au kwa Kamishna wa Wilaya.

Dar es Salaam,
8 Julai, 1982

A. M. A. OMARI,
Msajili wa Hati

TAARIFA YA KAWAIDA NA. 593

KUPOTEA KWA HATI YA KUMILIKI ARDHI

Sheria ya Uandikishaji wa Ardhi

(Sura ya 334)

Hati Nambari: 22157.

Miliki aliyeandikishwa: DOMINICO BAKALEMWA MWOLEKA, S.L.P. 391, Shinyanga.

Ardhi: Kiwanja Na. 97, Kitafu "Q" Shinyanga Mjini.

Eneo: Futi za mraba 5,500.

Taarifa imetolewa kwamba Hati ya Kumiliki Ardhi iliyotajwa hapo juu imepotea na ninakusudia kutoa hati mpya badala yake iwapo hakuna kipingamizi kwa muda wa miezi miwili tokea tarehe ya taarifa hii.

Hati ya asili ikionekana lazima irudishwe kwa Msajili wa Hati, Idara ya Hati za Ardhi, S.L.P. 1101, Mwanza.

Mwanza,
30 Juni, 1982 A. M. W. NYAKIHA,
Msajili Msaidizi Mwandamizi wa Hati

TAARIFA YA KAWAIDA NA. 594

KUPOTEA KWA HATI YA KUMILIKI ARDHI

Sheria ya Usajili wa Ardhi

(Sura ya 334)

Hati nambari: 24364.

Miliki aliyeandikishwa: AYUBU HAMIS IBRAHIM.

Ardhi: L.O. Na. 48617 Kiwanja Na. 508 Kitafu "N" kilichopo Bagamoyo Mjini.

Eneo: 300 Mita za Mraba.

Taarifa imetolewa kwamba hati ya kumiliki ardhi iliyotajwa hapo juu imepotea na ninakusudia kutoa hati mpya badala yake iwapo hakuna kipingamizi kwa muda wa miezi miwili tokea tarehe ya taarifa hii.

Hati ya asili ikionekana, lazima irudishwe kwa Msajili wa Hati za Ardhi, Idara ya Hati za Ardhi, S.L.P. 1191, Dar es Salaam, au kwa Kamishna wa Wilaya.

Dar es Salaam,
8 Julai, 1982

A. M. A. OMAR,
Msajili wa Hati

TAARIFA YA KAWAIDA NA. 595

KUPOTEA KWA HATI YA KUMILIKI ARDHI

Sheria ya Usajili wa Ardhi

(Sura ya 334)

Hati Nambari: 11325.

Miliki aliyeandikishwa: OMARI MUHAJI.

Ardhi: L.O. No. 16944, Kiwanja Na. 5, Kitafu "T" Dodoma Mjini.

Eneo: 5,159 Futi za mraba.

Taarifa imetolewa kwamba Hati ya Kumiliki ardhi iliyotajwa hapo juu imepotea na ninakusudia kutoa hati mpya badala yake iwapo hakuna kipingamizi kwa muda wa miezi miwili tokea tarehe ya taarifa hii.

Hati ya asili ikionekana, lazima irudishwe kwa Msajili wa Hati, Idara ya Hati za Ardhi, S.L.P. 1191, Dar es Salaam au kwa Msajili wa Hati Msaidizi, S.L.P. 1062, Dodoma au kwa Kamishna wa Wilaya.

Dodoma,
29 Juni, 1982

G. PANDUKA,
Msajili wa Hati

TAARIFA YA KAWAIDA NA. 596
KUPOTEA KWA HATI YA BIMA
NATIONAL INSURANCE CORPORATION OF (T)
LIMITED
(SHIRIKA LA BIMA LA TAIFA)
 HATI NA. L/167984 JUU YA MAISHA YA BWANA MUTAGWABA
 MUTALEMWA

Taarifa imetolewa kuhusu kupotea kwa hati ya bima iliyotajwa hapo juu nakala yake itatolewa kama malalamiko kupinga kutolewa kwa hati hiyo hayakuwakilishwa kwenye Shirika hili mwezi mmoja kuanzia tarehe ya tangazo hili.

S.L.P. 9264,
 Dar es Salaam,
 24 Juni, 1982

E. MWAKYAMI,
k.n.y. Meneja Mkuu

TAARIFA YA KAWAIDA NA. 597
KUPOTEA KWA HATI YA BIMA
NATIONAL INSURANCE CORPORATION OF (T)
LIMITED
(SHIRIKA LA BIMA LA TAIFA)
 HATI NA. L/173972 JUU YA MAISHA YA BWANA NARZIS
 H. KIHWILI

Taarifa imetolewa kuhusu kupotea kwa hati ya bima iliyotajwa hapo juu nakala yake itatolewa kama malalamiko kupinga kutolewa kwa hati hiyo hayakuwakilishwa kwenye Shirika hili mwezi mmoja kuanzia tarehe ya tangazo hili.

Dar es Salaam,
 23 Juni, 1982

E. MWAKYAMI,
k.n.y. Meneja Mkuu

TAARIFA YA KAWAIDA NA. 598
KUPOTEA KWA HATI YA BIMA
NATIONAL INSURANCE CORPORATION OF (T)
LIMITED
(SHIRIKA LA BIMA LA TAIFA)
 HATI NA. L/168085 JUU YA MAISHA YA BWANA MUTAGWABA
 C. D. MUTALEMWA

Taarifa imetolewa kuhusu kupotea kwa hati ya bima iliyotajwa hapo juu nakala yake itatolewa kama malalamiko kupinga kutolewa kwa hati hiyo hayakuwakilishwa kwenye Shirika hili mwezi mmoja kuanzia tarehe ya tangazo hili.

S.L.P. 9264,
 Dar es Salaam,
 24 Juni, 1982

E. MWAKYAMI,
k.n.y. Meneja Mkuu

TAARIFA YA KAWAIDA NA. 599
THE JUBILEE INSURANCE COMPANY LIMITED
(INCORPORATED IN KENYA)
OFISI KUU: P.O. BOX 30376, NAIROBI
KUPOTEA KWA CHETI CHA BIMA
 No. 23753 IN THE NAME OF MR. ZAHEER F. K. VISRAM

Maombi yametufikia kwa kutoa nakili nyingine ya cheti cha bima yenye nambari kama ilioko juu, tumepata habari kuwa cheti cha kwanza kimepotea au kuwekwa mahali pasipo julikana. Tangazo linatolewa yakuwa tusipopokea habari zozote kuhusu kupatikana kwa cheti hiki kwa muda wa siku thelathini kutufikia kwenye ofisi kuu ya shirika hili kuanzia tarehe ya tangazo hili, nakili nyingine itatolewa na ndiyo itakua kitambulisho kwa madhumuni ya maagano.

K. S. DAWOOD,
General Manager

TAARIFA YA KAWAIDA NA. 600
THE JUBILEE INSURANCE COMPANY LIMITED
(INCORPORATED IN KENYA)
OFISI KUU: P.O. BOX 30376, NAIROBI
KUPOTEA KWA CHETI CHA BIMA
 No. 20529 IN THE NAME OF MR. MOHAMED F. K.
 VISRAM

Maombi yametufikia kwa kutoa nakili nyingine ya cheti cha bima yenye nambari kama ilioko juu, tumepata habari kuwa cheti cha kwanza kimepotea au kuwekwa mahali pasipo julikana. Tangazo linatolewa yakuwa tusipopokea habari zozote kuhusu kupatikana kwa cheti hiki kwa muda wa siku thelathini kutufikia kwenye ofisi kuu ya shirika hili kuanzia tarehe ya tangazo hili, nakili nyingine itatolewa na ndiyo itakua kitambulisho kwa madhumuni ya maagano.

K. S. DAWOOD,
General Manager

TAARIFA YA KAWAIDA NA. 601
UTHIBITISHO NA USIMAMIZI WA MIRATHI
(Katika Mahakama ya Wilaya ya Tabora)
SHAURI LA MIRATHI NA. 1 LA 1981
Maombi ya barua za Usimamiaji wa Mirathi ya Sa'eh
Kulwa, marehemu
 Salumu Sa'eh, muombaji
TAARIFA YA KAWAIDA
(Kanuni ya 75)

Watu wote wanaodai kuwa na haki katika mirathi ya marehemu aliyetajwa hapo juu, wanafahamishwa kufika na kuangalia mashauri haya katika jalada kama wanaona inafaa kabla ya kutolewa kwa barua ya usimamiaji wa mirathi kwa mwombaji aliyetajwa hapo juu.

Mappingamizi yo yote kuhusu maombi haya yawe yameandikishwa mnamo au kabla ya tarehe 14 Agosti, 1981.

S.L.P. 63,
 Tabora,
 14 Mei, 1981

B. M. LUANDA,
Hakimu Mkazi
 Tabora

TAARIFA YA KAWAIDA NA. 602
UTHIBITISHO NA USIMAMIZI WA MIRATHI
(Katika Mahakama ya Wilaya ya Tabora)
SHAURI LA MIRATHI NA. 2 LA 1982
Maombi ya barua za Usimamiaji wa Mirathi ya Lameck
Sinda, marehemu
 Gideon Sinda, muombaji
TAARIFA YA KAWAIDA
(Kanuni ya 75)

Watu wote wanaodai kuwa na haki katika mirathi ya marehemu aliyetajwa hapo juu, wanafahamishwa kufika na kuangalia mashauri haya katika jalada kama wanaona inafaa kabla ya kutolewa kwa barua za usimamiaji wa mirathi kwa mwombaji aliyetajwa hapo juu.

Mappingamizi yoyote kuhusu maombi haya yawe yameandikishwa mnamo au kabla ya tarehe 21 Agosti, 1982.

S.L.P. 63,
 Tabora,
 21 Juni, 1982

B. S. MAGANGA,
Hakimu wa Wilaya
 Tabora

TAARIFA YA KAWAIDA NA. 603

UTHIBITISHO NA USIMAMIZI WA MIRATHI

(Katika Mahakama ya Wilaya ya Tabora)

SHAURI LA MIRATHI NA. 6 LA 1982

Maombi ya barua za Usimamiaji wa Mirathi ya Emmanuel G. Kiabo, marehemu

Marko G. Mgeleka, muombaji

TAARIFA YA KAWAIDA

(Kanuni ya 75)

Watu wote wanaodai kuwa na haki katika Mirathi ya marehemu aliyetajwa hapo juu wanafahamishwa kufika na kuangalia mashauri haya katika jalada kama wanaona inafaa kabla ya kutolewa kwa barua za usimamiaji wa mirathi kwa muombaji aliyetajwa hapo juu.

Mapingamizi yote kuhusu maombi haya yawe yameandikishwa mnamo au kabla ya tarehe 21 Agosti, 1982.

S.L.P. 63,
Tabora,
21 Juni, 1982

E. N. MASAWE,
Hakimu Mkazi
Tabora

TAARIFA YA KAWAIDA NA. 604

UTHIBITISHO NA USIMAMIAJI WA MIRATHI

(Katika Mahakama Kuu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dar es Salaam)

SHAURI NAMBA 6 YA MWAKA 1982

Maombi ya barua za Usimamiaji wa Mirathi ya Isaac Joseph Muyinga, marehemu

Euraliah G. Muinga, muombaji

TAARIFA YA KAWAIDA

(Kanuni ya 75)

Watu wote wanaodai kuwa na haki katika mirathi ya marehemu aliyetajwa hapo juu wanafahamishwa kufika na kuangalia mashauri haya katika jalada kama wanaona inafaa kabla ya kutolewa kwa uthibitisho wa Wasia wa mirathi kwa mwombaji aliyetajwa hapo juu.

Mapingamizi yoyote kuhusu maombi haya yawe yameandikishwa mnamo au kabla ya tarehe 26 mwezi wa Agosti mwaka wa 1982.

Wasia wa marehemu huyo aliyetajwa umewekwa amana na uwazi kwa upekuzi Mahakamani.

Imewasilishwa Dar es Salaam leo tarehe 25 mwezi wa Juni mwaka 1982.

J. P. LIPIKI,
Msajili

TAARIFA YA KAWAIDA NA. 605

UTHIBITISHO NA USIMAMIZI WA MIRATHI

(Katika Mahakama ya Wilaya ya Tabora)

SHAURI LA MIRATHI NA. 7 LA 1982

Maombi ya barua za Usimamiaji wa Mirathi ya Dr. Esrom J. Kerenge, marehemu

Apolonia K. Kerenge, muombaji

TAARIFA YA KAWAIDA

(Kanuni ya 75)

Watu wote wanaodai kuwa na haki katika mirathi ya marehemu aliyetajwa hapo juu wanafahamishwa kufika na kuangalia mashauri haya katika jalada kama wanaona inafaa kabla ya kutolewa kwa barua za usimamiaji wa mirathi kwa mwombaji aliyetajwa hapo juu.

Mapingamizi yote kuhusu maombi haya yawe yameandikishwa mnamo au kabla ya tarehe 7 Septemba, 1982.

S.L.P. 63,
Tabora,
9 Juni, 1982

B. M. LUANDA,
Hakimu Mkazi
Tabora

TAARIFA YA KAWAIDA NA. 606

UTHIBITISHO NA USIMAMIAJI WA MIRATHI

(Katika Mahakama Kuu ya Tanzania, Dar es Salaam)

SHAURI NAMBA 13 LA MWAKA 1982

Khatun Hamza Alavi au Khatun Alavi, marehemu

TANGAZO LA MAOMBI YA KUPIGA MUHURI TENA

(Kanuni ya 99)

Tangazo linatolewa kwamba maombi yameetwa katika Mahakama hii ya kupiga muhuri tena mirathi wa/ya marehemu wa Manchester aliyefariki Manchester tarehe 19 mwezi wa Aprili 1980 na Mahakama Kuu ya Manchester na maombi hayo yatasikilizwa katika mahakama hii na Jaji tarehe 3 mwezi wa Agosti mwaka 1982 wakati wa saa mbili na dakika arobaini na tano asubuhi.

Imewasilishwa Dar es Salaam leo tarehe 30 mwezi wa Juni mwaka 1982.

J. P. LIPIKI,
Msajili

TAARIFA YA KAWAIDA NA. 607

UTHIBITISHO NA USIMAMIAJI WA MIRATHI

(Katika Mahakama Kuu ya Tanzania Dar es Salaam)

SHAURI NAMBA 42 LA MWAKA 1982

Maombi ya barua za usimamiaji wa mirathi ya Lilyirmina Alexander Mosha, marehemu

Alexander Clemence Mosha, muombaji

TAARIFA YA KAWAIDA

(Kanuni ya 75)

Watu wote wanaodai kuwa na haki katika mirathi ya marehemu aliyetajwa hapo juu, wanafahamishwa kufika na kuangalia mashauri haya katika jalada kama wanaona inafaa kabla ya kutolewa kwa barua za usimamiaji wa mirathi kwa muombaji aliyetajwa hapo juu.

Mapingamizi yote kuhusu maombi haya yawe yameandikishwa mnamo au kabla ya tarehe 2 mwezi wa Agosti, mwaka wa 1982.

Wasia wa marehemu huyo aliyetajwa umewekwa amana na uwazi kwa upekuzi Mahakamani.

Imewasilishwa Dar es Salaam leo tarehe 12 Julai, 1982.

J. P. LIPIKI,
Msajili

TAARIFA YA KAWAIDA NA. 608

MAKAMPUNI YALIYOFUTWA KATIKA DAFTARI LA MAKAMPUNI

Sheria ya Makampuni

(Sura 212)

Inatolewa ilani chini ya kifungu 283 (3) cha Shera ya Makampuni kwamba Makampuni yafuatayo yatafutwa katika Daftari la Makampuni iwapo hapatatokea kipingamizi cho chote baada ya miezi mitatu kupita tokea tarehe ya ilani hii.

LOMBANK TANGANYIKA LIMITED.

MWANZA MEDICAL SUPPLIES CO. LTD.

KILIMANJARO WILD LIFE LIMITED.

NYANZA BREWERIES LIMITED.

D. T. HUTCHINS LIMITED.

SATHI ENGINEERING CONSTRUCTION CO. LTD.

Dar es Salaam,
10 Julai, 1982

R. B. MNGULWI,
Msajili wa Makampuni

TAARIFA YA KAWAIDA NA. 609

**JINA LA BIASHARA LILILOFUTWA KUTOKA
KATIKA DAFTARI LA MAJINA YA BIASHARA**

Sheria ya Uandikishaji wa Majina ya Biashara

(Sura 213)

Inatolewa ilani chini ya Kifungu 20 (3) cha Sheria ya Uandikishaji wa Majina ya Biashara, kwamba jina la biashara lililotajwa hapa chini limefutwa kuanzia tarehe 5 Julai, 1982.

TAHERY CLEARING AND FORWARDING HOUSE

Dar es Salaam,
15 Julai, 1982

R. B. MNGULWI,
Mtajili wa Majina ya Biashara

TAARIFA YA KAWAIDA NA. 610

HATI ZA UVUMBUZI

(Sura ya 217)

Inatangazwa kwa watu wote kwamba hati za uvumbuzi zenye maelezo yaliyomo kwenye Nyongeza ya Tangazo hili ziliandikishwa kuwa Nambari 2144 ya 1982 katika Daftari la Tanganyika la kuandikisha hati za uvumbuzi mnamo tarehe 6 mwezi wa Julai, 1982.

NYONGEZA

Nambari ya ombi: 2144.

Taraha ya ombi: 18 Juni, 1982.

Jina la muombaji: Ciba-Geigy Ag.

Anuani iliyoandikishwa: Basle, Switzerland.

Maelezo ya kukubaliwa katika Ulaya ya Uingereza:

Hati ya uvumbuzi Na. 1531260 ya 15/12/75 iliyotiwa mhuri tarehe 14/2/79 Uingereza.

Aina ya kitu kilichovumbuliwa: N-(Ortho-Substituted Benzyl Dinitrotrifluo-Romethly-Anilines and Compositions Containg them as Plant Growth Regulars.

Hati n.k. zilizowasilishwa kwenye masjala:—

1. Hati ya maanisho ya uvumbuzi iliyohakishwa Uingereza.
2. Hati ya Msimamizi Mkuu wa Uvumbuzi kutoka Uingereza.
3. Idhini ya wawakilishaji: Patma, c/o N.B.C., S.L.P. 9002, Dar es Salaam.

Dar es Salaam,
Juni, 1982

R. B. MNGULWI,
Mtajili wa Uvumbuzi

TAARIFA YA KAWAIDA NA. 611

DEED POLL DECLARING CHANGE OF NAME

Know all people by these presents that I the under-
signed SIMEON R. NYAMTEMA of Box 24 Kigoma Tanzania.

Lately called SIMEON R. NYAMTEMA do hereby abso-
lutely and utterly renounce, relinquish and abandon the

use of name SIMEON R. NYAMTEMA and adopt as from
the day of the date thereof the name of SHABANI R.
NYAMTEMA.

And for the purpose of evidance for such change of
name I hereby declare that I shall at all time thereafter
in all transaction matters and things whatsoever and
upon all ocassion use the subscribe the said name of
SHABANI R. NYAMTEMA in substitution for the said name
of so Renounced as aforesaid.

IN WITNESS WHEREOF I have here into signed my name
SHABANI R. NYAMTEMA and my assumed name SIMEON
R. NYAMTEMA.

This 11th day of March, 1982

S. R. NYAMTEMA,

the said SHABANI R. NYAMTEMA

Signed and delivered by

AND

In my presence this 11th March,
1982
Kigoma,

A. M. MBARUKU,
Senior District Magistrate

TAARIFA YA KAWAIDA NA. 612

MALI ISIYO NA MWENYEWU

(Katika Mahakama ya Wilaya ya Korogwe)

Sheria ya Jeshi la Polisi

(Sura ya 322—Kifungu 44)

Vitu vilivyoorodheshwa katika Jedwali hapa chini, vi-
likabidhiwa ama kuokotwa na Polisi. Mpaka sasa hakuna
dai lolote lililopokelewa kuhusu vitu hivi, kuwa kwa muda
wa miezi (6) sita kuanzia tarehe ya leo kama dai lo-
lote halitapokelewa vitauzwa kwenye mnada wa hadhara
na mapato yake yatashughulikiwa kisheria.

ORODHA

Na. ya Kiku

Maelezo ya mali

- | | |
|-------|--|
| 42/81 | Saa moja aina ya Cosmic mbovu. |
| 43/81 | Khanga pair tatu (3) nzuri. |
| 44/81 | Tairi moja ya gari L/Rover ya zamani. |
| 37/81 | Radio moja National bendi mbili, hand-
bag moja na suruali moja. Raba pair
mo'a, shuka moja, koti moja (vimecha-
kaa) sabuni za kufulia miche hamsini
na nne (54). |
| 38/81 | Shuka moja, tenge, shati mbili za mtoto,
suruali mbili za mtoto, kitambaa cha me-
za, kandambili za mtoto, pair moja vi-
mechakaa. |
| 28/81 | Matenge saba (7), Khanga nane, mifuko
mitatu (ya zamani). |
| 35/81 | Bomba mbili za maji za zamani. |
| 36/81 | Mapanga kumi na nne, shati mbili za mto-
to, nyundo moja, kofia moja na visu. |

S.L.P. 551,
Korogwe,
18 Juni, 1982

J. N. NIMKAZA,
Hakimu wa Wilaya Mwandamizi
Korogwe